TANGAZO LA SERIKALI Na. 866 la tarehe. 866

SHERIA YA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 16(1))*

SHERIA NDOGO YA MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA MJI WA MAFINGA YA MWAKA 2024

Jina

TS. Na. 211 la 2024

**1**. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga ya Mwaka 2024, na itasomwa pamoja na Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Mji wa Mafinga ya Mwaka 2024, ambayo katika Sheria Ndogo hii inarejewa kama “Sheria Ndogo kuu”.

Marekebisho ya kanuni ya 11

**2**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika kanuni ya 11-

(a) kwa kubadili mpangilio wa maudhui ya kanuni ya 11 kuwa kanuni ndogo ya (1);

(b) katika kanuni ndogo ya (2), kwa-

(i) kufuta alama ya nukta inayoonekana mwishoni mwa aya (f) na badala yake kuweka alama ya mkato; na

(ii) kuongeza mara baada ya aya ya (f) maneno ya kufungia yafuatayo:

“anatenda kosa”.

Marekebisho ya Jedwali la Kwanza

**3**. Sheria Ndogo kuu inarekebishwa katika Jedwali la Kwanza katika kipengele cha (2) cha Sehemu ya Kumi na Saba kwa kuongeza maneno “kwa ekari moja” mara baada ya kiasi cha “50,000/-”.

Dodoma,
29 Agosti, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi -OR-Tamisemi*